

Mwingiliano wa Kimtindo katika Tendi: Mifano kutoka *Mikidadi na Mayasa na Kalevala*

Jackson Ndung'u Mwangi, Nabea Wendo na Sheila P. Wandera-Simwa
Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya

Ikisiri

Uwepo wa tendi katika maeneo ya Afrika umezua mjadala na mgogoro mkali mno katika jamii ya usomi. Hii ni kutokana na rai kuwa wasomi na watafiti wengi kutoka maeneo ya Kimagharibi walidai kuwa Afrika hakuna tendi ila kinachodaiwa kuitwa tendi ni masimulizi ya kisifo tu. Wahakiki wengine wamezifutilia mbali tendi hizi kwa kudai kuwa maudhui yake ni ya kichawi na sihiri. Pia, vigezo vya kuainisha tendi vilivyotumiwa na wanazuo wa Kimagharibi vilikuwa vya kimaeneo na kimakusudi, walidhalilisha tendi za Kiafrika. Licha ya kuwa kuliibuka watafiti wa Kiafrika na kudai kuwa Kusini mwa Sahara ya Afrika kuna tendi, wao pia walielekea kutumia vigezo ambavyo ni vya kimaeneo. Ili kujaribu kutatua mzozo na utata uliopo kuhusu uwepo wa tendi katika maeneo ya Kiafrika, utafiti huu ulinua kuchunguza iwapo kuna mwingiliano wa kimtindo baina ya tendi za maeneo haya mawili. Madhumuni makuu yalikuwa kutathmini iwapo kuna mwingiliano wa vipengele vya kimtindo baina ya tendi za Kiafrika na zile za Kimagharibi licha ya tendi za Kiafrika kufutiliwa mbali na baadhi ya wasomi wa Kimagharibi. Makala yalichunguza tendi mbili zinazopatikana katika maeneo ya Kiafrika na Kimagharibi. Tendi hizi ni *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* unaopatikana Afrika na *Utendi wa Kalevala* unaopatikana Finland katika maeneo ya Kimagharibi.

Maneno Muhimu: Mwingilianomatini, Tendi, Mtindo, Ruwaza ya Shujaa.

Utangulizi

Mtindo katika fasihi hurejelea matumizi ya lugha. Lugha ya fasihi ni ya kihisia na hubeba dhamira ya mwandishi. Mbali na kuwasilisha ujumbe fulani, lugha ya fasihi humshawishi msomaji ili kujaribu kuathiri au hata kubadilisha msimamo wake. Ili kumwathiri msomaji kihisia na kimawazo, mwandishi hufinyanga lugha yake kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutumia tamathali za usemi; ambacho ni kipengele cha mtindo. Mbatiah (2001:13) ana maelezo kuwa fani ni

jumla ya vipengele vya kimtindo na kisanaa katika kazi ya fasihi vinavyojenga kionzi cha kubebea ujumbe na maana mahususi. Kwa hivyo, dhana ya fani ni mjumuiko mbalimbali wa vipengele vya kisanaa ambavyo huchangia katika ukamilifu wa kazi fulani. Maelezo haya yanaifanya dhana ya fani kuwa pana sana na ikiwa itashughulikiwa katika matini moja basi uchunguzi huo utakuwa na data kubwa.

Wamitila (2003) anadai kwamba fani ni jumla ya mbinu, mtindo na nyenzo anazotumia mwandishi kuiwasilisha dhamira na maudhui yake. Wamitila anaendelea kusema kuwa mwandishi hawezi kusema analotaka kulisema bila ya kutumia lugha. Lugha anayotaka kuitumia mwandishi pia lazima iwe na vikolezo au vitia ladha fulani. Kwa hivyo, mwandishi lazima ategemea fani.

Dhana ya mtindo katika kazi yoyote ile ya fasihi ina umuhimu wa kipekee kwani ni kigezo muhimu sana katika kukagua na kutathmini ubora wa kazi yoyote ile ya fasihi. Kwa vile kipengele cha kimtindo katika fasihi kina majukumu ya kipekee pia ni mojawapo wa kigezo bora cha kuchanganua, kulinganisha na kulinganua mwingiliano wa kazi mbalimbali za fasihi.

Mwingilianomatini ina umuhimu wa kipekee katika kazi ya fasihi kwani huonyesha ni kwa kiwango kipi vipengele kadha wa kadha vya kifasihi huilingiliana na athari zake katika kazi ya fasihi. Ili hadhira ya fasihi ielewe kazi yoyote ya fasihi, lazima ihusishe vipengele vingine nje ya muktadha wa usomaji au usimulizi ule. Alisema kuwa dhana ya kuingiza vipengele mbalimbali katika kazi ya fasihi ndiyo huitwa mwingilianomatini. Ili kutambua kama kweli kuna uhusiana kati ya tendi za Kimagharibi na zile za Kiafrika, utafiti huu ulinua kutathmini iwapo kuna mwingilianomatini wa kimtindo katika tendi za maeneo haya mawili. Surahii ilichunguza tendi mbili za Kiswahili kutoka maeneo ya Kiafrika na Kimagharibi ambazo ni *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* na *Kalevala* mtawalia. Tendi hizi zimechaguliwa kimakusudi kwani zinapatikana katika maeneo tofauti ulimwenguni, zimeandikiwa au kutafsiriwa kwa Kiswahili.

Sura hii iliongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini. Nadharia hii imepata kufasiriwa na kuhusishwa na wataalamu wengi kama vile De Saussure (1917), Kristeva (1969) na Bakhtin (1981). Saussure anafafanua suala la ishara katika lugha. Naye Bakhtin anajulikana kama mtaalamu aliyezua mtazamo mahsusi wa lugha uliosaidia wengine kuzua nadharia ya Mwingilianomatini. Tofauti na Saussure, Bakhtin alijihusisha na ishara katika lugha na jinsi zinavyoingana ili kuwa na maana. Hata hivyo, Julia Kristeva ndiye anayesifika kuwa mwanzilishi wa Nadharia ya Mwingilianomatini katika miaka ya sitini. Aliendeleza maoni ya Saussure kuhusu jinsi ishara hupata maana katika muundo, mtindo na fani katika matini na ya Bakhtin ya maneno na maana katika miktadha ya kijamii. Julia anaamini kuwa hamna matini yoyote ile ya kifasihi ambayo inaweza kuangaliwa kivyake au kujitegemea. Anasisitiza kuwa lazima kuwe na matini nyingine

inayohusiana nayo kwa mfano katika mtindo wa kiashiraji, katika matumizi ya sitiari, tashbihi, taswira na istiara, dhamira, maudhui, muundo wa msuko na usawiri wa wahusika.

Wamitila (2002) anasema kuwa kazi yoyote ile huwa na maana kwa sababu mambo fulani yanayohusiana nayo yamekwisha kuandikwa tayari. Kwa hivyo, upokezi na uelewaji wa utanzu kama utendi unategemea kuwako kwa utendi mwingine kabla ya utendi maalum kuchunguzwa. Alidai kuwa mwingiliano wa kati ya kazi mbili au zaidi huhusisha vipengele anuwai vya kimtindo na fani ambavyo hushirikisha mbinu za lugha, mbinu za kisanaa, wahusika, dhamira na hata maudhui. Nadharia ya Mwingilianomatini ina mihimili mbalimbali ikiwemo:

- a) Hamna matini yoyote ile ya kifasihi ambayo inaweza kuangaliwa kivyake au kujitegemea.
- b) Matini yoyote ile ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingi tangulizi.
- c) Kazi za kifasihi huundwa kutokana na mifumo ya kanuni na tamaduni mbalimbali zilizowekwa na kazi tangulizi za kifasihi ambapo taswira za maisha ya kawaida na uhusiano wa kimaana huunganishwa na kubadilishwa.
- d) Matini moja hufafanua usomekaji wa mkusanyiko wa matini zote za kongoo moja, ambapo matini tangulizi hufyonza na kujibiwa na matini mpya.
- e) Kila usomaji wa matini huwa ni kijalizo cha matini tangulizi na hivyo basi huigeuza.

Katika makala haya, watafiti alitumia njia ya kusoma na kuchanganua vitabu mbalimbali. Alisoma na kuhakiki tendi mbili za Kiswahili kutoka maeneo ya Kiafrika na Kimagharibi ambazo ni *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* na *Utendi wa Kalevala* mtawalia ambazo ndizo zilizotumika kama sampuli katika utafiti huu. Uhakiki huu hasa ulijikita katika masuala ya mwingiliano wa kimtindo baina ya tendi za maeneo ya Kiafrika na Kimagharibi. Pia, mtafiti alirejelea vitabu mbalimbali kwa minajili ya kufafanua hoja zake. Kamusi mbalimbali zilitumika pamoja na makala tofautitofauti zinazozungumzia ulinganishi wa kimtindo baina ya kazi mbalimbali za kifasihi. Mtafiti alisoma makala mbalimbali kwenye mtandao kuhusu mwingiliano wa kimtindo katika fasihi na sehemu ya nadharia.

Isitoshe, alisoma kazi mbalimbali ambazo zimeandikwa kuhusu Nadharia ya Mwingilianomatini kwa lengo la kuelewa zaidi kwa kuwa ni nguzo kuu katika kuchanganua dhana ya mwingiliano wa kimtindo katika fasihi.

Vipengele vya mwingiliano wa kimtindo katika Utendi wa Kalevala na Utendi wa Mikidadi na Mayasa

Katika sehemu hii, tumeangazia vipengele kadhaa: hadithi ndani ya hadithi, majibizano, majigambo, usimulizi na maigizo.

Hadithi ndani ya hadithi

Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, mtunzi anatumia vipengele anuwai vya kimtindo ili kufanikisha ujumbe wake. Mojawapo ya kipengele hiki ni matumizi ya hadithi ndani ya hadithi. Katika ubeti wa 12, mtunzi anaeleza kuwa katika kitabu kimoja cha hadithi alichokisoma, ndipo alipoipata hadithi anayoisimulia ambayo iliandikwa kwa lugha ya Kiarabu. Anadai kuwa hadithi yenyewe ilikuwa ya kiajabu, ya kuisimua na yenye mguso wa kipekee kwani ilishughulikia masuala mazito na yenye umuhimu wa kipekee katika maisha ya wanajami.

Mbwene hadithi kitabu

Hadithi iliyo ajabu

Yaandishwa Kiarabu

Njema mno ya ajaa.

Ubeti 12.

Anaianzisha hadithi yenyewe kwa kueleza na kujadili kuhusu Suwedi (babake Mikidadi) alivyokuwa tajiri na mwenye mali nyingi kupita kiasi. Hadithi yenyewe inasimulia historia ya awali kumhusu Suwedi na jinsi alivyofunga safari na kusafiri maeneo mbalimbali ilmuradi aweze kujichumia mali nyingi. Suwedi alipoaga dunia, inadaiwa kuwa mali yake yote ilitawanyika na aila yake ikaachwa bila chochote kwani Suwedi hakuwa hata na mke wa kuitunza mali yake. Hadithi hii inakuwa na umuhimu wa kipekee kwani ndiyo inaweka msingi wa masuala yote yanayozingira utendi mzima.

Katika *Utendi wa Kalevala*, dhana ya hadithi ndani ya hadithi inajitokeza kwa wingi mno. Katika ukurasa wa 23, Yokahani anakutana na Mwanamwini na kuanza kumhadithia jinsi siku za zama zilivyokuwa. Yokahani Anamweleza kuwa wakati nchi ilikuwa ikiumbwa, yeye kama shujaa alihusika katika uumbaji huo. Anaendelea kudai kuwa ana uwezo wa kipekee na ushujaa wake hauna kifani. Mwanamwini anaratali hadithi hii na kutambua kuwa kwa kweli, Yokahani hakuwepo wakati dunia ilikuwa ikiumbwa ila ni mwongo tu. Kwa ajili ya hiyo, Mwanamwini anamfanyia Yokahani sihiri na kumfanya aathirike hata zaidi.

Katika ukurasa wa 31, Aino (dadake Yokahani) anamweleza mamake yale yaliyomfika mwituni akitaifuta kuni kwa njia ya hadithi. Anadai kuwa akiwa mwituni, alikutana na Mwanamwini ambaye alijaribu kumrai waoane lakini alikataa. Anaendela kudokeza kuwa pete aliyopewa na Mwanamwini pamoja na nguo na vipuli vya dhamana kuu alizitupa na kumdhihirisha Mwanamwini kuwa kwa kweli hampendi. Hadithi hii inadhihirisha msimamo t habiti aliyokuwa nao

Aino na inatambulisha kuwa mwanamke katika jamii ya Kalevala amezinduka na ana uhuru wa kufanya maamuzi yake binafsi kuhusu masuala ya ndoa bila ya kushurutishwa.

Majibizano

Kama kipengele mojawapo cha kimtindo, majibizano yana nafasi na umuhimu wa kipekee katika Utendi wa Mikidadi na Mayasa. Katika ubeti wa 28 hadi 31, majibizano yanadhihirika pale ambapo wanaume wengi waliotoka mbali wakiwa wamebeba mali anuwai na kufika kwa Mayasa ili kumrai waoane. Walipofika nyumbani, walikutana na babake Mayasa (Jabiri) na kuanza kujibizana na kuumuliza kama ingewezekana wao kuoana na bintiye. Majibizano haya yanatambulisha utajiri wao na pia yanajaribu kuweka bayana mapendekezo na masharti ya Mayasa kwa atakayemuoa.

Wakamwambia Jabiri

Tujile tuna shauri

Tuna mali akthari

Tujile kutaka ndoa

Ubeti 28

Jabiri akawajibu

Nisikizani Waraabu

Mwanangu ana aibu

kwa hayo mlonambia

Ubeti 30

Majibizano haya yana umuhimu wa kipekee kwani yanatambulisha kuwa kwa kweli, Mayasa alikuwa ni kipenzi cha wengi, alikuwa mrembo kupindikia na alikuwa na msimamo thabiti. Pia, yanadhihirisha sifa tabia za babake za kuwa na tamaa kupindukia ya kumiliki mali.

Mikidadi alipokuwa akiwachunga kondoo wao na kutambua kuwa kulikuwa na kundi kubwa la wanaume waliofika nyumbani kwa Mayasa wakiwa wamebeba silaha, alitaka kujua nia yao ilikuwa ipi. Katika ubeti wa 66, anajibizana na mamake kuhusu suala hili. Tamima anamweleza kuwa watu wale walikuja kupigana na Mayasa kwani hakutaka kuolewa na watu walio na mali nyingi au wanaotambulika, ila alitaka tu mtu ambaye ni shujaa na ambaye angepigana naye na kumshinda katika vita.

Mamaye kamjibu

Hawale ni Waarabu

Wajire kumkhubu

Mayasa kuja muoa.

Ubeti 70

Na Mayasa hakukiri

Kuolewa na tajiri

Ila mshika khanjari

Ushujaa kumwelea

Ubeti 71

Baada ya majibizano haya, Mikidadi anaonyesha ujasiri kwa mamake na kumwambia kuwa liwe liwalo, angeenda kupigana na Mayasa, amshinde na amuo. Mazungumzo haya yanaishia kuwa na umuhimu wa kipekee katika maisha ya Mikidadi, kwani anachukua hatua ya kwenda kukabiliana na Mayasa na kutimiza azimio lake la kuwa shujaa tambulika katika nchi ile.

Katika *Utendi wa Kalevala*, suala la majibizano pia linabainika miongoni mwa wahusika mbalimbali. Baada ya Yokahani kufanyiwa uchawi na Mwanamwini, anajidharau sana na kuamua kwenda kumtafuta alipo ili alipize kisasi. Katika ukurasa wa 20, tunamwona Yokahani akijibizana moja kwa moja na mamake huku akidai kuwa ni lazima angefunga safari kwenda Vainola kukabiliana na Mwanamwini. Jambo hili linamkera mamake sana kwani alijua fika kuwa mwanawe akienda kupigana katika nchi ya ugenini na shujaa Mwanamwini, angefanyiwa sihiri na kuanganizwa.

*Kamwendea mama, mbele yake kasimama.
Nitakwenda vainola, kushindana Kalevala
Kamba mama hutaweza, baba amemkataza,
Yokahani kaambiwa: "Mwana utasihiriwa
Kile utaposafiri, utashindwakwa sihiri*

(Ukurasa 20)

Majibizano haya yanabainisha wazi kuwa Mwanamwini alikuwa shujaa wa kutambulika katika jamii hii ya Kalevala. Pia, yanaonyesha kuwa Mamake Yokahani alikuwa ni mtu wa kuwapa wanawe mawaidha na kuwatakiya mema. Inatambulika kuwa Yokahani alikuwa ni shujaa asiyewasikia wakuu wake jambo ambalo liliathiri maisha yake baadaye.

Majigambo

Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, ubeti wa 33, suala la majigambo linajitokeza kwani Jabiri anawaeleza wale wanaume waliofika kutaka kumuoa Mayasa kuwa bintiye ni mwenye maringo na hakutaka kamwe kuolewa na wanaume walio na mali nyingi au majina ya kutajika. Aliwaeleza kuwa Mayasa alikuwa akiringa tu juu ya farasi na alitaka kuolewa na mwanamume ambaye angekabiliana naye katika vita na kumshinda. Inadaiwa kuwa alikuwa akiupeperusha upanga juu hewani huku akijigamba jinsi alivyokuwa shujaa tambulika. Kwa mfano:

*Naye Mayasa aringa
Maidani kwa upanga
Na ambaye ajitenga
Akenda hatarejea.*

(Ubeti 33.)

*Husema akighani
Ali juu ya farasi
Wawapi mashuujaani
Watamanio kuo.*

(Ubeti 34.)

Katika *Utendi wa Kalevala* suala la majigambo linajitokeza sana hususan miongoni mwa mashujaa wengi wanaopatikana katika jamii hii. Baada ya Yokanani kukosa kusikiliza wosia wa mamake na kuamua kwenda kukabiliana na Mwanamwini akiwa na nia ya kumuoa, Mwanamwini anamteka nyara na kumfanyia sihiri na kumwacha Yokahani akiwa amelemaa. Ili kujiokoa kutoka hali ile, Yokanani anamwahidi Mwanamwini ahadi chungu nzima lakini

anajigamba tu huku akimdunisha Yokahani. Yokahani anaahidi kumpa Mwanamwini merikebu ili aachiliwe huru. Mwanamwini anajigamba huku akidai kuwa hana haja na merikebu yake kwani yeye ana jahazi nyingi mno zenye uganga na ambazo huenda bila matanga.

*Merikebu sina haja nayo, nina majahazi mia,
Majahazi ya uganga, huenda bila matanga,
Huenda yenyewe kweli, nina baburi na meli.
(Ubeti 25)*

Anapoendelea kuzama majini, Yokahani anaendelea kumrai Mwanamwini amuachilie huru huku akimwahidi kuwa ikiwa atamwachilia huru, atampa farasi wa kipekee. Mwanamwini anafutilia mbali pendekezo hilo na kuonyesha jinsi farasi wake alivyo wa kipekee na bora.

*Sikati wa mnyama. Nina wingi wa farasi,
weupe na weusi. Mchangani nina laki, farasi wako sitaki.*

Ukurasa 26

Yokahani anapomwahidi Mwanamwini dhahabu na fedha nyingi, Mwanamwini anaonekana kutothamini pendekezo hili na kujigamba kuwa yeye hahitaji fedha na mali yoyote kutoka kwa maskini kama Yokahani kwani ana vilima vingi vikubwa vilivyojaa fedha na dhahabu chungu nzima. Mifano hii inadhihirisha bayana kuwa kwa kweli tendi zote mbili zina wahusika ambayo wanadhihirisha suala la majigambo.

Usimulizi

Dhana ya usimulizi inajitokeza mno katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* na ina umuhimu wa kipekee wa kuelezea jinsi matukio mbalimbali yalivyotukia na kuathiri wahusika mbalimbali. Mtunzi anatusimulia kuhusu maisha ya Suwedi tangia utotoni mwake. Inadaiwa kuwa Suwedi alikuwa ni mtu mwenye mali nyingi na mfanyibiashara mashuhuri aliyesafiri nchi mbalimbali akishiriki biashara za aina mbalimbali. Inasimuliwa kuwa hali hii ya Turadi kupenda kusafiri ilifanya mali yake kutawanyika na kumpotea kwani hata hakupata wakati wa kuo mke wa kumsaidia kulinda mali yake. Jambo hili lilimfanya Mikidadi kuishia kuwa maskini hohehahe na kuishia kwenda kwa mjombawe kutafuta kazi ya kufuga wanyama. Usimulizi huu unatupatia historia ya familia ya Mikidadi na inatueleza kilichosababisha Mikidadi kuishia kuwa maskini.

Baada ya Mikidadi kupigana na Mayasa na kumshinda, tunasimuliwa jinsi Jabiri alivyokuwa akitumia hila ili Mikidadi na Mayasa wasioane. Inadaiwa kuwa Jabiri alikuwa mwenye tamaa kupita kiasi ya mali na alimdharau Mikidadi kwa vile alikuwa maskini. Anapanga hila na waliokuwa kwenye kikao na kumwekea mahari ya kiwango cha juu sana ili ashindwe kuilipa. Pia, tunasimuliwa kuwa

Jabiri alitaka kutumia hila na kujaribu kukataa kumpa Mikidadi pete baada ya makubaliano ili akikawia kuleta mahari, auvunje ule mkataba.

Katika *Utendi wa Kalevala*, kuna matumizi ya usimulizi. Katika ukurasa wa 10, Tunasimuliwa jinsi Mwanamwini alivyozaliwa. Inadaiwa kuwa matukio yaliyoandamana na kuzaliwa kwake yalikuwa ya kiuhalisiaajabu na ya kuogofya. Inasimuliwa kuwa mamake Mwanamwini (Bikira Binti Hewa) alikuwa ni mrembo kupindukia, alikuwa msichana aliyeumbika na aliishi maisha ya utukufu. Inadaiwa kuwa alisukumwa na upepo mkali mno hadi katika bahari kubwa kule ambako alishika mimba na tumbo lake likavimba na kuwa kubwa ajabu. Inadokezwa kuwa mimba ya mwanamke huyu ilimchukua miaka mia tisa ili Mwanamwini azaliwe. Mazimulizi haya yanaonyesha upekee wa maisha ya Mwanamwini na kudhihirisha kuwa kwa kweli, alikuwa kiumbe mwenye sifa za kipekee na za kustaajabisha.

Maigizo

Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, dhana ya maigizo imejitokeza na ina umuhimu katika kukuza na kuendeleza dhamira pamoja na maudhui katika utendi wenyewe. Katika kuonyesha weledi wake katika vita, Mayasa anadhihirisha dhana ya maigizo kutokana na hali ambayo anapambana na wanaume waliokuja kujaribu bahati ya kumuoa. Inadaiwa kuwa alipowaona wale wanaume, alipanda juu ya farasi wake huku akipiga kelele na kupeperusha upanga juu ya hewa. Alizunguka kila mahali akidai kuwa mwanamume atakayemuoa ni sharti wapataane katika ndoa. Maigizo zaidi yanajitokeza pale ambapo Mayasa anawaegema wale wanaume huku akidhihirisha weledi wake wa kivita. Katika ubeti wa 60, Mayasa anaonekana akiwaua wanaume wengi na idadi kubwa ya waliobaki inakimbia mbio sana ikihofia maisha yao. Jambo hili linaonyesha kuwa kwa kweli, Mayasa alikuwa shujaa wa kutajika.

*Wakamwegema kwa panga
Mayasa akazikinga
Hadi mbele akasonga
Hata kuwakurubu.*

Ubeti 59

*Hawale wataka ndoa
Ikawa kupinduliwa
Mayasa akiwaua
Wengi wakamkimbia*

Ubeti 60

Mifano ya maigizo haya inadhihirisha kuwa kwa kweli, Mayasa alikuwa na weledi wa kipekee wa kupigana na yanatambulisha kuwa hata wanawake wana uwezo wa kukabiliana na wanaume katika vita licha ya kudhalilishwa na wanaume katika jamii. Maigizo pia yanajitokeza pale ambapo Mikidadi anadhihirisha weledi wake wa kivita anapokabiliana na Mayasa. Inadokezwa kuwa Mikidadi alitumia mbinu zozote zile za kivita na mwishowe aliweza kumpiku na kumshinda Mayasa. Pia, akiwa jangwani kutafuta mahari, maigizo anuwai yanadhirika hususan wakati anakabiliana na maadui wake huku akiwapokonya mali yao.

Katika *Utendi wa Kalevala*, dhana ya maigizo inadhihirika miongoni mwa wahusika wakuu. Katika ukurasa wa 71, maigizo yanadhihirika kutokana na jinsi ambayo Limarini anatafuta madini ya kutengeza sampo. Anaonekana akienda mwituni kutafuta madini ambayo inamchukua zaidi ya siku tatu kuipa. Baada ya kupata ile madini, anakutana na Ng'ombe ambaye hatoi maziwa na kumuua kwa nyundo yake huku akivunjavunja shingo lake na kuikatakata nyama zake huku akizirusha motoni. Anapoitengeneza sampo, anadhihirisha jinsi sampo yenyewe inavyosaga sayiri na kutoa chumvi kwa wakati mmoja.

Mifano hii inabaini kuwa kwa kweli, kuna mwingilianomatini wa vipengele mbalimbali vya kimtindo baina ya *Utendi wa Kalevala* ambao unapatikana maeneo ya Kimagharibi na *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* unaopatikana maeneo ya Kiafrika.

Hitimisho

Katika makala haya, imebainika wazi kuwa kuna uwezekano wa kazi mbili za fasihi kutoka maeneo tofauti ya kijiografia kuathiriana na kuingiliana kwa kiwango fulani. Kwa muda mrefu, kumekuwa na mjadala mkubwa sana hususan kutoka kwa wanazuo wa Kimagharibi waliofutulia mbali uwepo wa tendi katika maeneo ya Kiafrika. Wengi wao walidai kuwa zile zinazodaiwa kuitwa tendi ni masimulizi tu ya kisifo ambayo hayajaafiki kuitwa tendi. Pia, imedhihirika kuwa kuna vipengele vingi sana vya kimtindo na kifani vinavyoingiliana baina ya tendi za Kimagharibi na zile za Kiafrika. Baada ya kuchanganua *Utendi wa Kalevala* unaopatikana maeneo ya Kimagharibi na *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* unaopatikana maeneo ya Kiafrika, imebainika kuwa kuna baadhi ya vipengele vya kimtindo ambavyo vinaingiliana baina ya tendi hizi mbili kama vile hadithi ndani ya hadithi, masimulizi, majigambo, maigizo na dayalojia.

Marejeleo

- Allen, G. (2000). *Intertextuality*. London: Routledge.
- Bakhtin, M. M. (1981). *The Dialogic Imagination*. Texas: University of Texas
- Barthes R. C. (1967). *The Death of The Author*. Columbia: Readers printing press.
- Barthes, R. (1981). *The Theory of Text. Untying the Text: A Post Structural Reader*. New York: University of Colombia.
- Christener, T. (2013). *J. M Coetzee's Occluded Intertextuality: Reading Text, Intertext and the Archieve in Life and Time of Michael K and Foe*. Vancouver: University of British Columbia.
- Deme, M. K. ((2009). *Heroism and the Supernatural in the African Epics Towards a Critical Analysis*. Michigan: Western Michigan University.
- Campbell, J. (1949). *The Hero With Thousand Faces*. Novato: New World Library.
- Finnegan R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Clarendon: Oxford University Press.

- Folley, J. M. (1990). *Traditional Oral Epic*. Berkely: Los Angeles.
- Gamme, J. G. (1981). *On the Intention of and Sources of Daniel 1-IV*. Vt. 31/3
- Gordord, B. (1993). *Intertextuality in Encyclopedia of Contemporary Literary Theory: Approaches, Scholarly Terms*. Toronto: University of Toronto Press.
- Harlan, L. (2003). *The Goddesses. Gender in Indian Hero Worship*. Peak Printing press. New York.
- Heinman (1972). *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Nairobi: East Africa publishers Limited.
- Jago, M. (2007). *The Fiction of Chinua Achebe*. London: Palgrave.
- Kehinde, A. (2003). Intertextuality and the Contemporary African Novel. *Nordic Journal of African studies*.
- Kristeva, J. (1984). *Revolution in poetic Language*. Columbia: Columbia University Press.
- Kristeva, J. (1986). *The Kristeva Reader Blackwell*. Oxford: Oxford University Press.
- Mbatiah, A. M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and publishing.
- M'ngaruti, T. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mulokozi, M. M. (1988). *Tanzu za Fasihi Simulizi katika Mulika na 21*. Dar es Saalam: TUKI. Uk 1-24.
- Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahii*; OSW 105. Dar es Saalam: Chuo kikuu cha Huria cha Tanzania.
- Mulokozi, M. M (1997). *Utendi wa Nyakiiru Kibi*. Morogoro: ECOL Publication.
- Mushenyezi, A. (2003). *Twentieth Century Literary Theory*. Kampala: Makerere University Press.
- Nagy, G. (2006). *Epic hero; a Companion to Ancient epic*. Washington: Harvad Online Publication, Center for Hellenic Studies.
- Njogu, K. na Wafula, R. M. (2007). *Nadharua za Uhakiki wa Kifasihi*: Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Ogunpita, S. A. (2007). *Genotext and Intertext. The Grammatology of a Literary idiolect*. California: California linguistic Publication.
- Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa Lugha ya Fasihi*: Dar es Saalam: KAUTTU.
- Symour, C. (1978). *Story and Discourse: Narrative Structure in Fiction and Film* Cornell University Press: Ithaca.
- Timothy, L. (2009). *New Perspectives in Campbells Monomyth Theory*. New Jersey: Princeton University Press.
- TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*: Dar es Saalam: TUKI
- Udumukuwu, O. (2006). *Novel and change in Africa*. Port Harcourt: University of port Harcourt press.

- Odumukuwu, O. (2007). *Nigeria Literature in English; Emerging Critical Perspectives. M and J. Communication*. Nigeria: Port Harcourt.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi; Msingi wa Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Video Muwa Publishers Ltd. Nairobi.
- Eriki, T. (2011). *Intertextuality in the Cinematic Production of Quentin Tarantino*. Masaryk University. Faculty of Arts. Phd thesis.
- Foss, T. (2005). *The Heroic Spheres: Creating and Applying a Model to Define and Categorise Literary Heroes*. Harvard University Phd thesis.
- Lynne, H. (2012). *Intertextuality Interventions in the Novel of Marlene Streeruwitz and Lilian Faschinger*. University of Nottingham. Phd thesis.
- Mathew, G. (2009). *Gilgamesh the Giant: The Qumran Books of Giants. Appropriation of Gilgamesh Motifs*. Florida State Universty. Phd Thesis.
- Michaux, G. (2003). *Gilgamesh and Homer: a Comparative Study of Motifs Sets, Distinctions and Similarities*. Open Universitet. Antwerpen. M.A. Thesis.
- Richie, B. (2006). *Templates of Intertextuality in the Modern African Novel: A Study of Chinua Achebe's Things Fall Apart and Ayi Kwei Aima's The Beutiful One Are Not Yet Born*. Mouloud Mammer University. Faculty of Arts. Phd Thesis.
- Tinah, M. A. N. (2012). *Harmonization and Intertextuality in Translating Shakespeare Sonnets into Metrical Arabic poetry*. Ar- Najah National University. M.A thesis.
- Uzoechi, N. (2012). *Intertextuality and the Truth of Achebe's Fiction: Militarised Nigeria Post Colony in Anthill of Savannah*. University of Ibadan. Phd thesis.